Victims Services
Attorney General & Justice

Hati ya Haki za Wahanga

(Sheria ya Msaada na Haki za Wahanga ya 2013)

Swahili/Swahili

Kama wewe ni mhanga wa tendo la jinai, unakuwa na haki. Haki hizi zinaitwa Hati ya Haki za Wahanga. Hivi ndivyo inavyosema:

Heshima

Utashughulikiwa kwa heshima, hadhi na huruma. Utamaduni wako utaheshimiwa wakati wote.

Taarifa kuhusu huduma

Utaambiwa upesi iwezekanavyo kuhusu huduma mbalimbali zinazoweza kukusaidia, zikiwemo ushauri nasaha na huduma za kisheria.

Upatikanaji wa huduma

Kama unahitaji msaada wa kimatibabu, ushauri nasaha, na wa kisheria utaweza kuupata ikiwa unapatikana.

Taarifa kuhusu upelelezaji wa kosa la jinai

Kama ukiuliza, utaambiwa kuhusu maendeleo ya upelelezaji wa polisi. Lakini kwa baadhi ya kesi zinaweza kuwa na vitu vichache ambavyo polisi wanashindwa kukuambia.

Taarifa kuhusu uendeshaji mashtaka

Uendeshaji mashtaka unahusishwa na kumpeleka mkosaji mahakamani kwa tendo la jinai. Hii inafanywa na polisi, au, kwa kesi kali, Mkurugenzi wa Mashtaka wa Serikali.

Kama Mhanga, utaambiwa:

- mashtaka ni nini AU kwa nini mkosaji HAJAshtakiwa;
- hukumu yoyote ya uendeshaji mashtaka kubadilisha au kuacha mashtaka;
- tarehe na mahali pa usikilizaji wa kesi mahakamani;
- matokeo ya mwisho ya mahakama, ikiwemo kukata rufaa yoyote au hukumu ya kufungwa jela iliyotolewa.

Kama uendeshaji mashtaka unafikiria kubadilisha au kuacha mashtaka utaelezewa kama kosa la jinai:

- lilikuwa kosa la kijinsia, AU
- limekusababisha madhara ya kimwili, kiakili au kisaikolojia.

LAKINI, uendeshaji mashtaka hauhitaji kuongea nawe kama:

- hutaki kuiongelea, AU
- hupatikani.

Taarifa kuhusu kuwa shahidi

Kama unahitaji kutoa kielelezo cha ushahidi wakati kesi inavyosomwa utaambiwa kesi itafanyika VIPI na NINI utatakiwa kufanywa.

Hakuna mawasiliano na mkosaji

Wakati kesi yako inakuwepo mahakamani utazuiwa kufanya mawasiliano na mkosaji na mashahidi wa mkosaji.

Kuhifadhi usiri wako

Unaweza kuweka anuani na nambari zako za simu ziwe siri isipokuwa mahakama inasema tofauti.

Mambo ya mahakama kabla ya kesi kusomwa

HUPASWI kuenda kwenye usikilizaji wa upelekaji (kama daawa ndogo) au mambo mengine ya mahakama kabla ya daawa ISIPOKUWA mahakama inakulazimika kufanya hivyo.

Kurudishwa kwa vifaa vyako vilivyotumiwa kama vielezo vya ushahidi

Kama polisi au uendeshaji mashtaka umechukuwa vifaa vyako kama vielelezo vya ushahidi ni haki yako kurudishiwa upesi iwezekanavyo.

Ulinzi wako

Kama unahitaji ulinzi waambie polisi au uendeshaji mashtaka wakati mkosaji anaomba dhamana.

Sharti maalum la dhamana

Utaambiwa kuhusu masharti yoyote maalum ya dhamana aliyopewa mkosaji, ambayo yanakusudia kukulinda wewe au familia yako, kama sharti linalosema ni marufuku kwa mkosaji kuwasiliana na wewe.

Uamuzi wa dhamana

Kama ulikuwa mhanga wa shambulio la kijinsia au shambulio lingine kali utaambiwa ikiwa kama mkosaji atapewa dhamana au la.

Maelezo ya matokeo ya mhanga

Kwa baadhi ya kesi unaweza kuiambia mahakama kuhusu namna kosa la jinai lililokuathiri na utapewa msaada na ufadhili kufanya hivi. Hii inaitwa kutoa ‘maelezo ya matokeo ya mhanga.”

Wakati mkosaji anapoachwa huru

Kama mkosaji umefungwa jela unaweza kuambiwa kama mkosaji utaachwa huru hivi karibuni, ametoroka jela au ameachwa huru kwa siku moja.

Wakati mkosaji anaomba ahadi ya mfungwa kutotoroka

Unaweza kutoa oni ikiwa mkosaji wako anaomba ahadi ya mfungwa kutotoroka.

Msaada wa kifedha

Kama umejeruhiwa kutokana na matokeo ya tendo kubwa la jinai la binafsi, unaweza kustahiki kupata msaada wa kifedha.

Taarifa kuhusu taratibu za malalimiko

Unaweza kutoa malalamiko kama unadhani haki zako chini ya Hati hazijatendewa na unaweza kuuliza kupata taarifa kuhusu namna ya kufanya hivi.

Ikiwa wewe ni mhanga wa tendo la uhalifu unakuwa na haki.

Pigia simu Njia ya Upatikanaji kwa Wahanga kwa kutumia nambari 1800 633 063 ili kupata taarifa na msaada.

Hati ya Haki za Wahanga

Huko New South Wales kuna Hati ya Haki za Binadamu ili kulinda na kukuza haki zako kama wewe ni mhanga wa tendo la jinai. Hati hiyo inahusika na idara zote za serikali ya NSW. Pia inahusika na mashirika yoyote yasiyo ya kiserikali na wakandarasi (isipokuwa maofisa binafsi wa serikali na wataalamu wa udaktari), waliofadhiliwa na Jimbo ambalo linatoa msaada kwa wahanga. Hati inasema jinsi unavyotakiwa kutendewa na kusaidiwa kama unakuwa mhanga wa tendo la jinai. Hati imeingizwa kwenye *Sheria ya Msaada na Haki za Wahanga ya 2013*.

Nani ni mhanga wa tendo la jinai?

Kwenye *Sheria ya Msaada na Haki za Wahanga ya 2013*, mhanga ni mtu ambaye anayeathirika na madhara kutokana na matokeo ya moja kwa moja ya kosa la jinai.

Ninaweza kufanya nini kama nadhani haki zangu chini ya Hati hazitendeki?

1. Unapaswa kuongea na yule mtu unayeshughulika naye kuhusu matatizo. Mara nyingi matatizo yanaweza kutatuliwa kwa namna hiyo.
2. Kama bado hujaridhika, ni haki yako kumuuliza yule mtu kukuambia namna ya kuandikisha malalamiko kwa idara yao. Idara inapaswa kupanga watafsiri au msaada mwingine utakaohitajika. Unaweza kupata msaidizi wa kukusaidia kuandikisha malalamiko. Huyu anaweza kuwa rafiki au mfanyakazi.
3. Kama bado hujaridhika baada ya malalamiko yameshaangaliwa na idara unaweza kuwasiliana na Huduma kwa Wahanga. Kazi yao ni kukusaidia na malalamiko yako na kukuambia kitu gani kinachoweza kufanyika kuhusu hiyo.

Maelezo ya mawasiliano

Simu 1800 633 063
Eneo la jiji la Sydney ..... (02) 8688 5511
Njia ya Mawasiliano kwa Wananchi wa Asili 1800 019 123
Faksi ..... (02) 8688 9632
Muda wa Kazi ..... saa 2 As. mpaka saa 12 jioni, Jumatatu mpaka Ijumaa (isipokuwa siku kuu)
Barua pepe ..... vs@agd.nsw.gov.au
Tovuti ..... www.lawlink.nsw.gov.au/vs
Tumia anuani hiyo kwa barua zote ..... The Commissioner, Victims Services, Locked Bag 5118, Parramatta NSW 2124

© Jimbo la New South Wales kwa njia ya Huduma kwa Wahanga, Idara ya Mwanasheria Mkuu na Haki, Juni 2003. (UCHAMBUZi Julai 2013). Hati hii inaweza kutolewa nakala kwa ajili ya nia binafsi, za elimu na za serikali. Ruhusa lazima ipatikane kutoka kwa Idara kwa ajili ya matumizi yote nyingine.

Miundo mbadala ya taarifa hii inapatikana.

Hati hii iliandaliwa na Huduma kwa Wahanga kwa ajili ya utoaji wa taarifa za jumla.

ISBN 978 1 922121 29 5 (FS10m • 07/2013)